# MAFUNZO YA KAMATI YA KITAALAMU YA DAWA WILAYA YA ULANGA

VIGEZO VYA KUANZISHA MADUKA YA DAWA MUHIMU

# VIGEZO VYA KUANZISHA MADUKA YA DAWA MUHIMU…

1. Watumishi
2. Eneo
3. Jengo la DLDM
4. Mkataba

# VIGEZO VYA KUANZISHA MADUKA YA DAWA MUHIMU

1. Watumishi

- Fundi Dawa Sanifu – Diploma (Pharmaceutical Techn)
- Fundi Dawa Sanifu Msaidizi – Cheti (Pharmaceutical Asst.)
- Muuguzi au Mkunga (Nurse or Nurse Midwife)
- Tabibu (Clinical Officer)
- Tabibu Msaidizi (Asst. Clinical Officer)

# Watumishi.......

- *Licha ya kuwa na elimu na ujuzi wa msingi ulioanishwa hapo juu, yeyote anayetaka kuwa mtoa dawa katika DLDM atalazimika kupitia mafunzo ya utoaji dawa yatakayoidhinishwa na Mamlaka kwa kipindi maalumu kama itakavyopangwa*

# VIGEZO VYA KUANZISHA MADUKA YA DAWA MUHIMU…

2. Eneo

- Yeyote anayetaka kufungua DLDM, wakati wa kupeleka maombi yake ataonyesha wazi mahali duka hilo litakapokuwa na anuani kamili ya sehemu hiyo.
- Duka la Dawa Muhimu halitaruhusiwa kuwa katika jengo lolote ambalo ndani yake kunauzwa na kunywewa pombe

# Eneo…

Nivyema ikafahamika kuwa:

- Mamlaka inayoshughulikia maombi hayo ina uwezo wa kukataa kuanzishwa kwa Duka sehemu yeyote isiyokubaliana nayo kwa sababu maalum.
- Pia mamlaka inayotoa kibali cha kuanzisha DLDM ina uwezo wa kumshauri muombaji kufungua duka lake sehemu nyingine ili kupunguza msongamano wa maduka na pia kutoa huduma katika sehemu ambazo hazina huduma hii

# Eneo...

- Kwa nia ya kutaka dawa zitolewe kwa usahihi zaidi baada ya mgonjwa kuonwa na mganga, uidhinishaji wa DLDM utatoa upendeleo maalumu kwa maduka yanayotaka kufunguliwa karibu na zahanati au vituo vya afya.

# Eneo...

- Kwa sehemu za katikati ya mji, maduka haya yanapaswa kuwa umbali wa mita 300 kati ya duka na duka jingine.
- Kwa sehemu za gulio/ soko yanapaswa kuwa na umbali wa mita 200
- Pia yanapaswa kuwa mita 500 toka ilipo pharmacy.
- Hata hivyo, idadi ya watu itazingatiwa ili kulete uwiano wa maduka na watumiaji wa huduma

# Eneo.....

- ANGALIZO:
- Pamoja na maelezo hayo hapo juu, TFDA inaelekeza kuwa maduka yafunguliwe kwa kila kata kwanza, hadi kata zote zitakapo pata maduka, na vivyo hivyo kwa kila kijiji.
- Baada ya kila kata na kijiji kuwa vimepata maduka, ndipo vigezo vya umbali nilivyovitaja hapo juu vitakapotumika.

# VIGEZO VYA KUANZISHA MADUKA YA DAWA MUHIMU…

3. Jengo la DLDM

- Liwe la kudumu na imara
- Liwe na nafasi ya kutosha ili kuweza kufanya shughuli za kutoa dawa, kutunza dawa na kuuza bila taabu
- Liweze kuzuia kuingia na kuwepo kwa wadudu waharibifu (panya, mende, popo n.k).

# Jengo la DLDM….

- Liwe na stoo yenye rafu au mbao za chini na mzunguko mzuri wa hewa
- Liwe na sakafu imara inayoweza kusafishwa kwa maji na kemikali za kuua wadudu
- Liwe na sehemu maalumu au nafasi ya kuweza kutoa ushauri na maelezo faragha kwa wagonjwa (siyo kufanya matibabu)
- Liwe na chumba maalumu au kabati inayofungika kwa ajili ya kuweka dawa za daraja la kwanza (part I drugs)
- Vyumba viwe vimepakwa rangi nyeupe au rangi nyingine inayong’aa inayoweza kusafishwa kwa maji

# Jengo la DLDM....

- Liwe na mlango, dirisha imara na ikiwezekana kuwe na nondo
- Liwe na angalau vyumba viwili (chumba cha kutolea dawa kiwe na ukubwa wa kutosha ( km ft. 10 kwa futi 9 na kimo cha kwenda juu ft 8)

- (kama hakuna bomba la maji Kuwepo na maji salama basi maji ya ndoo na beseni la kunawia litafaa pia)
- Mazingira ya kuzunguka jengo yawe katika hali ya usafi wakati wote

# VIGEZO VYA KUANZISHA MADUKA YA DAWA MUHIMU...

4. Mkataba

- Mwenye Duka la Dawa Muhimu na mtoa dawa watabidi wasaini mkataba ambao utaelezea masharti ya kazi na majukumu ya kila mmoja wao.
- Nakala ya Mkataba huu utawasilishwa na kutunzwa kwa Katibu wa DDTC.

# MAFUNZO YA KAMATI YA KITAALAMU YA DAWA WILAYA YA ULANGA

- THANK YOU FOR YOUR ATTENTION

- THE END